Uendelezaji Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma

Imewasilishwa na;
Idara ya Uendelezaji Rasilimaliwatu,
Ofisi ya Rais,
Menejimenti ya Utumishi wa Umma,
S.L.P. 2384,
DAR ES SALAAM.

Yaliyomo

1. Utangulizi,
2. Jukumu la uendelezaji Rasilimaliwatu,
3. Jitihada zilizochukuliwa katika kuwaendeleza watumishi,
4. Utekelezaji,
5. Changamoto,
6. Tufanye nini?,
7. Matarajio,
8. Hitimisho.

1.0 Utangulizi

- Watumishi ni Rasilimali ya msingi katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu na malengo ya Serikali katika ngazi ya Taasisi na Taifa kwa ujumla,
- Nguvu na mafanikio ya Taasisi yoyote na Taifa lolote inategemea aina ya watumishi waliopo kwenye Taasisi au Taifa husika,
- Kwa msingi huo hawana budi kuendelezwa ili waweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

Utangulizi …

- Usemi huu unasisitizwa pia na Serikali kupitia Mipango, Sera na miongozo mbalimbali iliyotolewa kuhusu umuhimu wa kuwaendeleza watumishi ili waweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo,
- Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za mwaka 2009 Kanuni G.1 (4), (7) – zinasisistiza Taasisi za Umma kujenga watumishi wenye uwezo ili kutoa huduma kwa matarajio ya wananchi; kwa kuzingatia mahitaji halisi ya mafunzo ikiwa ni pamoja na kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili hiyo.

Utangulizi …

- Kanuni 103 (1-6) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003 – inaagiza kwamba ni jukumu la kila mwajiri kuwaendeleza watumishi wake kwa kuzingatia matokeo ya tathmini ya mahitaji ya mafunzo na programu sahihi ya mafunzo ili kuwapatia watumishi ujuzi unaostahili kutekeleza majukumu yao ya sasa na ya baadae.

Utangulizi …

- Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma, toleo la 2 ya mwaka 2008 kifungu 4.8 inasisitiza kwamba, kwa nia ya kuendeleza na kuimarisha ujuzi wa watumishi, vyombo vyote vya umma vinatakiwa kuwa na programu ya mafunzo na maendeleo kulingana na mpango wao wa utumishi.

Utangulizi …

- Mpango wa Pili wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini Tanzania 2010/11-2014 (MKUKUTA – II) uliopangwa kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, unasisitiza suala la kujenga uwezo wa rasilimali watu kiujuzi, kimaarifa na upangaji na matumizi mazuri ya Rasilimaliwatu kuwa ni moja ya njia muhimu ya kuliwezesha Taifa kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo 2025.

Utangulizi …

- Umuhimu wa kuwaendeleza watumishi kila wakati haukwepeki. Unahitaji kutekelezwa ili kuwawezesha watumishi hao kuwa nguvu na injini ya Serikali katika kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kuzingatia mazingira yaliyopo.

2.0 Jukumu la Uendelezaji Rasilimaliwatu

Uendelezaji wa Rasilimaliwatu ni hatua ya kuwapatia watumishi ujuzi, maarifa au uelewa unaohitajika ili kuwawezesha kufanya kazi kwa Ufanisi. Katika utumishi wa umma jukumu hili hili linasimamiwa na kuratibiwa na OR-MUU kupitia Idara ya Uendelezaji wa Rasilimaliwatu kwa:-

- Kuandaa Sera na miongozo mbalimbali inayohusu mafunzo na kusimamia utekelezaji wake, ikiwa ni pamoja na kuratibu nafasi za mafunzo kutoka kwa nchi na jumuiya rafiki/wadau wa maendeleo.

Jukumu la Uendelezaji …

- Kujenga uwezo wa Taasisi za utumishi wa umma kufanya tathmini za mahitaji ya mafunzo na kuandaa programu za mafunzo.

3.0 Jitihada zilizochukuliwa kuwaendeleza watumishi

3.1 Maandalizi ya sera na miongozo

a) Sera ya Mafunzo imekwisha andaliwa na kupitishwa na Kikao cha Baraza la Mawaziri na hivi sasa iko katika Tovuti ya OR-Muu.

b) Waraka wa Utumishi Na. 5 wa Mwaka 2011 kuhusu Mafunzo Elekezi ya Awali kwa Watumishi Wapya, umeandaliwa ukiwa ni marekebisho ya Waraka Na. 4 wa mwaka 2005.

Jitihada …

- Waraka Na. 5 wa mwaka 2011 unasisitiza:
  - Watumishi wanaoajiriwa kwa mara ya kwanza wapatiwe mafunzo elekezi ya awali ndani ya kipindi cha miezi mitatu tangu kuajiriwa.
  - Waajiri wote wahakikishe kwamba watumishi wapya wanapopatiwa mafunzo elekezi ya awali pia wafanyiwe upekuzi.
  - Waajiri wote wanapaswa kutenga fedha kwenye bajeti ya kila mwaka kwa ajili ya mafunzo haya.

Jitihada …

- Mafunzo elekezi ya awali yatatolewa na Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania (TPSC), Chuo cha Serikali za mitaa (LGTI) na Chuo cha Uongozi wa Mahakama (IJA).

- Mafunzo elekezi ya awali yanawawezesha watumishi wapya kuuelewa Utumishi wa Umma na kufahamu misingi yake, sheria kanuni na taratibu za utendaji kazi na kuwajengea utendeji kazi bora, maadili, nidhamu uadilifu na ustahimilivu.
- Kwa msingi huo, suala la utekelezaji wa Waraka Na. 5 wa mwaka 2011 kuhusu Mafunzo Elekezi ya Awali kwa Watumishi wapya linapaswa kupewa kipaumbele.

3.2 Kujenga uwezo wa Taasisi kufanya tathmini ya mahitaji ya mafunzo

- OR-MUU kupitia PSRP imeendelea kutilia mkazo suala la kuwawezesha watumishi wa umma kiutendaji kwa kuwapatia mafunzo yanayozingatia mahitaji yao na malengo ya Taasisi.

- Hili limefanyika kwa kuziwezesha Wizara, Idara zinazojitegemea, wakala na Sekretariati za mikoa kufanya tathmini ya mahitaji yamafunzo na kuandaa mipango sahihi ya mafunzo inayozingatia mahitaji halisi ya mafunzo.

Jitihada …

- Tathmini ya mahitaji ya mafunzo ni mchakato unaolenga katika kuziwezesha Taasisi kutambua mapungufu ya kiujuzi, kiutaalam na kitaaluma waliyonayo watumishi na kuainisha sifa na ujuzi wanaotakiwa kuwa nao ili kufikia malengo yaliyopangwa na hatimaye kuandaa mipango halisi ya mafunzo.

Jitihada …

Tathmini ya mahitaji ya mafunzo inaziwezesha taasisi:-

- Kuoanisha mafunzo yanayotolewa na mpango mkakati wa Taasisi husika pamoja na matokeo ya upimaji utendaji kazi.
- Kutambua mahitaji ya rasilimaliwatu yanayostahili kupewa kipaumbele kwa ajili ya utekelezaji wa dira, dhima na malengo ya Taasisi,
- kuwa na matumizi yenye tija kwa kuwekeza rasilimali chache zilizopo katika mafunzo ambayo yanahitajika (value for money),
- Kuandaa mipango ya mafunzo inayozingatia mahitaji.

Jitihada …

3.3 Uratibu wa fursa za Mafunzo kutoka kwa Wadau wa Maendeleo

- OR-MUU imeendelea kufanya jitihada za kuhakikisha upatikanaji na uratibu wa fursa za mafunzo ya muda mfupi na mrefu kutoka kwa wafadhili.
- Aidha Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma inashiriki katika kubainisha aina ya fursa za mafunzo hayo kwa kuzingatia vipaumbele na mahitaji ya kitaifa.

Jitihada …

- Baada ya kupata fursa hizo huzitangaza kwenye magazeti na tovuti ya utumishi **www.utumishi.go.tz** na nyingine kuzipeleka kwenye Taasisi husika ili waweze kuteua watumiaji.

Jitihada …

- Serikali za nje ambazo kwa kiasi kikubwa zinasaidia kutoa fursa za mafunzo ya muda mrefu na mfupi ni: Ubelgiji, Uholanzi, Australia, Jamhuri ya Korea, Ujerumani, China, Japan, India, Malaysia, Italia, Indonesia, Misri, Singapore, Malaysia, Sweden, na Jumuiya ya Madola,
- Watumishi walionufaika na fursa za mafunzo ktoka kwa wadau wa maendeleo kati ya mwaka 2012/13 - 2013/2014 ni kama ifuatavyo:-

2009/10 - 2013/14

MFADHILI	WALIOPATA 2009/10		WALIOPATA 2010/11		WALIOPATA 2011/12		WALIOPATA 2012/13		WALIOPATA 2013/14		JUMLA
	F	M	F	M	F	M	F	M	F	M	
Ubeligiji	72	72	108	109	-	-	-	-	124	60	545
Korea ya Kusini	73	35	92	24	80	36	50	66	21	34	511
Japan	104	28	78	26	84	36	43	133	94	28	654
Australia	7	7	11	11	12	30	30	46	27	38	219
India	38	79	41	83	106	54	133	155	99	52	840
Jumuiya ya Madola	100		80		91		-	-	-	-	271
China	86	60	172	101	285	199	105	222	5	3	1,238
Uholanzi	68	79	81	84	-	-	61	100	72	96	641
JUMLA KUU	**548**	**360**	**663**	**438**	**658**	**355**	**422**	**722**	**442**	**311**	**4,919**

4.0 Utekelezaji wa Programu za mafunzo/mafunzo Elekezi

- Katika utekelezaji wa Awamu ya Pili ya PSRP (2008 – 2012) Wizara 16, Idara Zinazojitegemea 16, Wakala tano na Sekretarieti za Mikoa 10 ziliwezeshwa kufanya tathmini ya mahitaji ya mafunzo na kuandaa mipango ya mafunzo.
- Nafahamu pia kwamba katika utekelezaji wa LGRP Mamlaka za Serikali za Mitaa karibu zote ziliwezeshwa kufanya tathmini ya mahitaji ya mafunzo na kuandaa mipango halisi ya mafunzo kwa watumishi wake. Je mipango hiyo mnaitekelezaje?.

4.1 Sekretarieti za Mikoa

2012/13 hadi 2013/14 (Programu za Mafunzo)

Sekretarieti ya Mkoa	Watumishi waliopangwa Katika mpango	Watumishi waliopata Mafunzo	% ya Utekelezaji
Simiyu	26	10	38
Morogoro	21	61	290
Geita	54	16	27
Rukwa	6	6	100
Lindi	89	89	100
Pwani	35	0	0
Kagera	82	56	68
Singida	115	49	43
Arusha	31	27	87
Katavi	21	0	0
DSM	11	11	100

2012/13 hadi 2013/14 (Mafunzo Elekezi)

Sekretarieti ya Mkoa	Watumishi Wapya	Waliopata Mafunzo Elekezi	Wasiopata Mafunzo Elekezi	% ya Utekelezaji
Simiyu	136	0	136	0
Morogoro	107	45	62	42
Njombe	180	0	180	0
Geita	83	83	0	100
Rukwa	26	0	26	0
Lindi	65	16	49	25
Pwani	37	0	37	0
Kagera	76	76	0	100
Singida	76	0	76	0
Arusha	81	31	50	38
Katavi	44	0	44	0
DSM	8	0	8	0

4.2 Mamlaka za Serikali za Mitaa

2012/13 hadi 2013/14 (Programu za Mafunzo)

Mamlaka za Serikali za Mitaa	Watumishi waliopangwa Katika mpango	Watumishi waliopata Mafunzo	% ya Utekelezaji
Nyasa -DC	115	43	37
Mvomero -DC	752	187	25
Singida - DC	40	12	30
Mtwara - MC	106	241	227
Magu -DC	148	108	72
Tunduru - DC	112	112	100
Newala – DC	135	92	68
Karagwe - DC	120	82	68
Kilombero - DC	185	178	96
Lindi - DC	140	28	20

2012/13 hadi 2013/14 (Mafunzo Elekezi)

Mamlaka za Serikali za Mitaa	Watumishi Wapya	Waliopata Mafunzo Elekezi	Wasiopata Mafunzo Elekezi	% ya Utekelezaji
Nyasa - DC	330	330	0	100
Mvomero - DC	490	434	56	86
Singida - DC	240	0	240	0
Mtwara - MC	241	241	0	100
Magu -DC	333	36	297	11
Tunduru - DC	281	0	281	0
Newala – DC	333	35	298	11
Karagwe - DC	318	0	318	0
Kilombero - DC	343	365	22	106
Lindi - DC	184	99	85	54

5.0 Changamoto

Kama tulivyoona kwenye mifano iliyotolewa hapa juu:-

- Bado suala la uendelezaji watumishi kwa baadhi ya Sekretarieti na Mamlaka za Serikali za Mitaa halipewi kipaumbele cha kutosha katika mipango ya taasisi na kutengewa bajeti, kutekelezwa na kufanyiwa tathmini.
- Baadhi ya Taasisi huchukulia kwamba suala la uendelezaji wa watumishi ni kitu cha kufanyika wakati bajeti itakaporuhusu.
- Baadhi ya waajiri kutoweka wazi fursa za mafunzo zinazowasilishwa kwao kutoka kwa wadau wa maendeleo.

Changamoto…

- Baadhi ya watumishi kuomba nafasi za mafunzo ambazo haziendani na mahitaji yao halisi,
- Watumishi kuahirisha mafunzo yanayotolewa na wafadhili dakika za mwisho na kusababisha fursa hizo kupotea na kuleta usumbufu.

6.0 Tufanye nini?

- Suala la kuendeleza watumishi ni la lazima na muhimu lipewe umuhimu wa pekee na liwe ni moja ya kipaumbele cha Taasisi wakati wa kutayarisha bajeti. Tuweke mikakati ya kuhakikisha kwamba mipango ya mafunzo inatekelezwa ipasavyo.
- Mipango ya mafunzo ipitiwe mara kwa mara na ihuishwe sambamba na mipango mikakati ya Taasisi ili isipitwe na wakati.
- Fursa za mafunzo zitumike ipasavyo. Watumishi wanapopata fursa hizo wasisitizwe kuzitumia

Tufanye nini? …

Kuhusu mafunzo elekezi ya awali kwa watumishi wa umma:

- Kuna haja ya kuhakikisha kwamba watumishi ambao hawajapelekwa mafunzo haya wanapelekwa na wale watakaoajiriwa wapatiwe mafunzo haya ndani ya miezi mitatu tangu kuajiriwa.
- Waajiri wahusike katika kuhimiza mafunzo elekezi ya awali ikiwa ni pamoja na kutoa ushauri pale unapohitajika na kufuatilia utekelezaji

Tufanye nini? …

- Ili waajiri waweze kufahamu mafunzo haya yanatolewaje, OR-MUU itaendelea kuvihimiza vyuo vilivyopewa jukumu la kuendesha mafunzo haya vitoe ratiba ya mafunzo haya kila mwaka itakayopelekwa kwa waajiri ili kutoa msukumo wa utekelezaji wa mafunzo haya.

7.0 Matarajio

- Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma inatarajia kuendelea kutoa miongozo na kuweka mifumo na usimamizi mzuri wa kuwaendeleza watumishi.

8.0 Hitimisho

- Kimsingi utumishi wa umma hauwezi kuwa na watumishi bora wenye upeo wa kutekeleza majukumu yao kufikia malengo ya kitaasisi na kitaifa kama mapungufu yao ya kiutendaji na ya kiujuzi hayatatafutiwa ufumbuzi.
- Aidha mafunzo elekezi kwa watumishi wapya ndiyo silaha pekee ya kuwa na watumishi wa Umma wenye uelewa wa pamoja kuhusu utumishi wa umma, na wenye maadili katika utendaji kazi.

Hitimisho …

- Naomba nisisitize na kutoa wito kwenu washiriki kama wasimamizi wa rasilimaliwatu katika sehemu zenu za kazi kuhakikisha kwamba program zenu za mafunzo zinatekelezwa ipasavyo.
- Vilevile kuhakikisha kwamba watumishi wote ambao hawajapewa mafunzo elekezi wanapatiwa mafunzo hayo ndani ya miezi mitatu tangu kuajiriwa.

Hitimisho …

- Aidha kutokana na jukumu tulilonalo la kusimamia maagizo mbalimbali yanayotolewa na Serikali Kuu, tuhakikishe kwamba Mamlaka/Sekretarieti za Mikoa zinatoa kipaumbele katika mipango yao kwa kutenga fedha za mafunzo elekezi na ya kuwaendeleza watumishi katika bajeti zao hata kwa kutumia vyanzo vya ndani kwa ajili ya watumishi walio chini yao.

A S A N T E N I K W A K U N I S I K I L I Z A